# Zana Za Uzalishaji wa Viazi: Mwongozo wa Mafunzo kwa Wakulima na Wataalam wa Ugani Afrika Mashariki

**Abstract:**

Mwongozo huu unatoa mwelekeo na mbinu bora za kilimo na aina ya zana na mashine zinazopa- tikana katika kuongeza uzalishaji wa viazi wenye tija. Watumiaji na au walengwa wa mwongozo huu ni wakulima wadogo wanaojihusisha na uzalishaji wa zao la viazi, ufugaji na watoa huduma wa trekta. Mwongozo huu unazingatiamabadiliko ya tabianchi, na matumizi sahihi ya zana zinazofaa katika uzalishaji bora wa viazi. Baadhi ya mashine zilizoelezwa/kujadiliwa ni zile zilizo chini ya mra- di wa kuendeleza matumizi ya zana bora katika kilimo “Africa Agricentre of Excellence (AAE)” un- aotekelezwa na asasi zifuatazo; Kibaigwa Flour Supplies Ltd nchini Tanzania na Tinga nchini Kenya kwa kushirikiana na muungano wa sekta binafsi ya makampuni matatu ya Ujerumani ya Grimme, Pottinger na Bayer AG. Mwongozo huu ni kitendeakazi kitakachomsaidia mtumiaji kupata maarifa ya ziada ambayo yatasaidia kuainisha miongozo mingine ya mafunzo juu ya uzalishaji wa viazi vya chakula. Kwa hivyo, haimaanishi kuwa Mwongozo huu utumike peke yake.